

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Musoma)

Simu: 028-2622560/2622550

Fax: 028-2620550

E-mail: md@musomamc.go.tz

Website: www.musomamc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa ya Musoma,
S.L.P. 194,
MUSOMA.

Tarehe 4/9/2018

TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma Bi. Fidelica G. Myovella ana utaarifu umma kuwa Mwenge wa Uhuru unatarajiwa kupokelewa katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma mnamo tarehe 7/9/2019 saa 1:30 asubuhi Stendi ya Mabasi Bweri.

Mbio za Mwenge zinatarajiwa kufungua, kutembelea na kuweka mawe ya msingi katika miradi 5 yenye thamani ya Tsh. Bil.1,998,687,063.74.

Miradi itakayofikiwa na Mwenge ni pamoja na ufunguzi wa vyumba 3 vya madarasa na ofisi ya Walimu katika Shule ya Msingi Kamarage 'B', Ufunguzi wa Madarasa mawili katika shule ya Baruti Sekondari, Uzinduzi wa Kiwanda cha uchenjuaji wa Madini ya dhahabu FRAMAL investment Limited.

Vilevile miradi mingine ni uwekaji jiwe la Msingi katika hospitali ya CF pamoja na kutembelea Mradi wa kitalu Nyumba kilichopo Kata ya Buhare.

Aidha mkesha wa Mwenge wa Uhuru utafanyika katika viwanja vya shule ya Sekondari Mwisenge.

Wananchi wote wanaombwa kujitokeza kwa wingi na kushangilia Mwenge wa Uhuru katika maeneo yote utakapopita.

Imetolewa na,

Mafuru M. Mafuru

Afisa Habari/Uhusiano

Manispaa ya Musoma